

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**PHONE NO.0653222972  
0763553984**

**SHULE YA SEKONDARI IKAPU  
S. L. P 359,  
TUKUYU.**

**KUMB. NA. BDC/S.3383/JI/VOL1 /14**

10/12/2020

**NDUGU.....**

**S.L.P.....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKAPU KWA  
MWAKA WA MASOMO 2021.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Nina furahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ikapu mwaka 2021. Shule ipo katika kijiji cha Mbambo kata ya Kambasegela karibu na mpaka kati ya halmashauri ya wilaya ya Rungwe na Busokelo. Shule ipo Kilometa 14 kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Busokelo barabara kuu iendayo Ipinda -Kyela. Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/1/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 7/1/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/1/2021.

**2.0 MANDHARI:**

Shule ina mazingira ya kuvutia. Nyasi fupi, maua na miti ni sehemu ya vivutio hivyo. Upepo mwanana kutoka bwawa la asili la Ikapu husaidia kurekebisha hali ya joto la eneo la shule yetu.

**3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

Wakati wa kujiunga ,mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

**3.1 SARE ZA SHULE:**

**a) Wasichana;**

- (i) Blauzi/shati mbili (2) za mikono mifupi.
- (ii) Sketi mbili (2) ndefu zenye rinda kubwa "**DAMU YA MZEE ILIYOKOLEA NA NYEUSI**" sketi fupi haziruhusiwi kuvaliwa.
- (iii) Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vyenye sifa ya kupakwa kiwi na vyenye kisigino kifupi na view vya kufunga kamba. Uje pia na raba kwa ajili ya michezo.
- (iv) Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (2)
- (v) Nguo za michezo rangi ya bluu (truck suit na fulana)

**b) Wavulana:**

- (i) Mashati mawili (2) meupe kitambaa cha tetron mikono mifupi
- (ii) Suruali mbili (2) zenye linda mbili tu. Suruali moja iwe rangi ya “**DAMU YA MZEE ILIYOKOLEA NA NYINGINE IWE NYEUSI**” Ni marufuku kushona mtindo wa jinsi na suruali za kubana yaani modo haziruhusiwi.
- (iii) Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vyenye sifa ya kupakwa kiwi na vyenye kisigino kifupi na view vya kufunga kamba. Pia uje
- (iv) Soksi nyeusi jozi mbili (2)
- (v) Nguo za michezo rangi ya bluu(truck suit,bukta na fulana). Uje pia na raba kwa ajili ya michezo.

**3.2 MICHANGO YA CHAKULA**

- (i) Mahindi yaliyokobolewa yajae ndoo ya lita 10
- (ii) Maharage kimbo 5 kwa muhula
- (iii) Chumvi mifuko miwili (2)
- (iv) Mafuta ya kula lita moja
- (v) Shilingi 5000 kumlipa mpishi.

**3.3 VIFAA VYA USAFI NA ELIMU YA KUJITEGEMEA.**

Unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo: Jembe lenye mpini, kwanja, ndoo ya lita 10 na panga.

**3.4 BIMA YA AFYA:**

Ili kuhakikisha mwanafunzi anasoma bila matatizo yoyote ya kiafya, ni lazima kuwa na bima ya afya. Ni wajibu wa mzazi kumkatia bima mtoto wake.

**3.5 VIFAA VYA KUJIFUNZIA:**

Unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kujifunzia.

- (i) Kalamu ya wino (pen) rangi ya blue au nyeusi pamoja na kalamu ya risasi (pencil).
- (ii) Daftari kumi(10) three quire
- (iii) mkebe wenye vifaa (mathematical set) mmoja(1)
- (iv) Rula moja (1) yenye vipimo
- (v) Faili la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
- (vi) Kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili (Dictionary).
- (vii) Bunda moja la karatasi (Ream) ukubwa wa  $A_4$

#### **4.0 SHERIA, KANUNI NA MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.**

##### **4.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

- (i) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na kila mtu aliyemzidi umri au anayefanana naye.
- (ii) Mwanafunzi anatakiwa awajibike katika shughuli zote ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- (iii) Mwanafunzi atambue kuwa ana wajibu kuwa kusoma ndiyo kazi iliyomleta hapa shuleni na kushindwa kusoma na kujifunza kwa bidii ni dhambi kubwa kwake.(iv) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni kila siku na kuhudhuria vipindi vyote kikamilifu.
- (iv) Mwanafunzi afahamu mipaka ya shule na ajue kuwa hatakiwi kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa.
- (v) Kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (vi) Kuvaa sare ya shule kama inavyotakiwa.
- (vii) Kuzingatia ratiba ya shule muda wote.
- (viii) Kutunza mali za uma.

##### **4.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI**

- (i) Kuwa na simu shuleni au kutumia simu akiwa shuleni bila ruhusa toka kwa walimu
- (ii) Uwizi
- (iii) Ubakaji (fornication)
- (iv) Matumiziya marijuana(bangi), cocaine, heroine,etc
- (v) Kutumia kileo (drunkenness)
- (vi) Kosa la jinai, kupigana na kugomaadhabu.
- (vii) Kuharibu /kupoteza mali ya shule.
- (viii) Kutotii Wimbo / bendera yaTaifa.
- (ix) Kuwa na mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba

DYSON CHIBONA  
**MKUU WA SHULE**

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA 2021

1. Jina kamili .....
2. Mahali alipozaliwa .....
3. Tarehe ya kuzaliwa .....
4. Jina la baba .....hai/marehemu..... kama ni  
mzima, anafanya kazi gani? ..... nambayasimu .....
5. Jina la mama ..... hai/marahemu.....kama  
nimzima, anafanyakazi gani? ..... namba ya simu.....
6. Je mama na baba wanaishi pamoja? ..... kama hapana; Je, wewe  
unaishi na nani? .....
7. Kama yatima jina la mlezi.....kazi anayofanya.....  
namba ya simu.....uhusianonamlezi.....
8. Anwani ya mzazi /mlezi .....
9. Shule ya msingi uliyotoka .....
10. Dhehebu/ Dini .....
11. Nathibitisha kuwa habari nilizotoa ni za kweli na sahihi.

Saini ya mwanafunzi ..... Tarehe.....

Saini ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

*Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule unaporipoti shuleni.*

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

STUDENT NAME.....

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

- 1. Vision with glasses right ..... left.....
- 2. Blood pressure .....
- 3. Hemoglobin .....
- 4. F. V. Bleeding .....
- 5. Urine for sugar. ....
- 6. Stool for routine examination .....
- 7. Venereal diseases .....
- 8. Neurosis .....
- 9. T. B. Test .....
- 10. Any abnormality
  - a) Heart .....
  - b) Lung .....
  - c) Spleen .....
  - d) Chest .....
- 11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes .....

Doctor's name.....

Signature and official stamp

.....

Date .....